

# Kulifumbua Fumbo la Dunia Yao na Dunia Yetu

K. W. Waliaula

*Ikisiri*

Unapoisoma riwaya hii ya 'Dunia Yao' ya Said A. Mohamed, mwanzo kabisa huna budi kujiuliza dunia yao, nani hao? Halikadhalika, utajiuliza kama ipo dunia yao, je sharti pawepo kinyume chake? Na kinyume cha dunia yao kinachoashiriwa lakini bila kutajwa moja kwa moja ni nini? Je, ni dunia yangu au dunia yetu? Yaani, je, kama kuna dunia yao basi yamkini pana dunia yetu au dunia yangu? Kutafakari juu ya dunia hizo kunaibua fikira za wao, na sisi, na mimi. Dunia yao nani hao? Dunia yetu sisi nani? Dunia yangu, mimi nani? Haya ndiyo masuala yanayomkanganya msomaji sambamba na yanavyoelekea kumkanganya Ndi—mhusika mkuu wa Said Mohamed. Makala haya yanajaribu kuyapatia majibu maswali haya na yanayofanana nayo.

## 1.0 Utangulizi

Huwezi kuisoma *Dunia Yao* ya Said A. Mohamed bila kuhisi kwamba unakabiliwa na fumbo la kufumbua, tena fumbo lenye utata. Kama msomaji huna budi kujiuliza maswali mengi kuhusu ufumbuzi wa fumbo hilo, sio tu kwamba fumbo la dunia yao linaweza kufumbuliwa, bali pia wewe mwenyewe unaweza kulifumbua. Mara nyingine utahisi moyo unakupapa kama msimulizi Ndi— wa riwaya hii apendavyo kusema—moyo unakupapa kwa vile hii si hadithi ya kawaida ya paukwa pakawa yenye msuko sahili na wahusika wa kawaida, hadithi inayoweza kueleweka na hata watoto wa chekechea. *Dunia Yao*, ipo katika dunia yake ya ubunifu na usomaji na fasiri. Inataka mikakati tofauti ya usomaji katika kuifumbua na kufichua kina cha maana yake. Dunia ya *Dunia Yao*, imekitwa kwenye mantiki tofauti, mantiki iliyo kinyume na mantiki ya hadithi zilizozoeleka.

## 2.0 Dunia za Ferdinard Oyono na Said A. Mohamed

Je, kuna tofauti kati ya "dunia" za Ferdinard Oyono na Said A. Mohamed? Jibu la swali hili ni ndiyo na hapana. Mhusika Baklu, ambaye ni dobi wa Mzungu katika riwaya ya Oyono iliyotungwa katika mandhari ya enzi ya ukoloni wa Mfaransa nchini Kameruni ndiye anayetoa kauli kuhusu dunia mbili, dunia yake ya watu weusi wanaomenyeka chini ya utawala katili wa Mfaransa, kwa upande mmoja, na dunia ya Mtawala huyo Mfaransa kwa upande mwingine. Baklu anamwelezea kauli hiyo mhusika mkuu na msimulizi Toundi, mweusi mwenzake ambaye anaelekea kutoelewa vizuri hali halisi ya pengo lililopo kati ya dunia yao, weusi na dunia ya watawala wao, weupe. Baklu anaelekezea nathari, sio kwenye mambo yanayofanana, bali yale yanayotofautiana katika dunia hizo mbili na kuzifanya ziwe kinzani moja kwa nyingine. Dunia hizi zinadhihirika kwa kile mwanafalsafa Olufemi Taiwo angekiita "*metaphysics of*

*difference*” metafizikia ya utofauti. Kwanza dunia hizo zinatofautiana kwa waliomo ndani; moja ina watu weupe, nyingine watu weusi ambapo rangi ya ngozi imepewa kipaumbele. Pili, zinatofautiana kwa yaliyomo ndani, yanayoruhusiwa, na kulazimishiwa kuwa ndani na mielekeo ya waliomo ndani kuhusu hayo yaliyomo. Kuhusu dunia yao akina Baklu, yaani dunia ya weusi, kuna heshima, uchanya, maajabu, na uchawi. Hatuwezi kuelewa maana ya heshima hapa hadi tuilinganishe dunia hii ya weusi na dunia ya weupe, ambayo badala ya heshima haina siri. Yaani heshima anayoizungumzia Baklu inahusiana na kuyafanya siri mambo mengi; kutoonyeshana mahaba hadharani au kutofanya ngono hadharani. Heshima na siri zimefungamana katika dunia ya weusi. Labda hili linaeleweka zaidi ukizingatia kwamba miaka mingi baada ya uhuru bado ni mwiko kuzungumzia ngono kwa uhuru kwingi barani Afrika, hata kama vitendo vya ngono navyo vinafungamana sana na idadi kubwa ya watu wanaofariki barani.

Kile ambacho si rahisi kukikatia kauli ni kama kutaja “maajabu” na “uchawi” ni kipimo cha Baklu cha kile anachokiona kama kasoro zilizopo katika dunia yake na wenzake weusi. Hayo ndiyo maneno ambayo Raphael Kahaso na Nathan Mbwele, watafsiri wa tafsiri ya Kiingereza ya riwaya ya Oyono iliyoandikwa kwa Kifaransa, wanayatumia katika kutafsiri maneno *mystery* na *magic*. Kutafsiri *mystery* kama “maajabu” kunaweza kuwa sawa lakini kutafsiri *magic* kama “uchawi” si sawa kwa sababu uchawi linabeba kivuli cha maana hasi na hivyo, halielekei kufanana na maana ya neno la lugha ya awali. Aidha, ni vigumu kuuona msimamo wa Baklu kama ule wa kuiponda dunia yake, ilhali matumizi ya “uchawi” hapa yanaelekea kuiponda na kuikosoa dunia hiyo. Baklu anasisitiza zaidi “heshima” ya dunia yake na anailinganisha dunia hii yenye heshima na ile ya weupe yenye ukosefu wa heshima. Japo Baklu hasemi moja kwa moja kwamba dunia ya weupe haina heshima, tunabaini hilo kwa kutaja kwake heshima kuambatana na dunia ya weusi na kuonyesha kutokuwa siri na kwa mambo ya siri kwa upande wa dunia ya weupe kama ishara ya kutokuwepo heshima.

Kama vile “dunia” ya Said A. Mohamed, “dunia” ya Oyono hapa haimaanishi sayari bali jumla ya mtazamo na mkabala wa kimaisha, kifikra, na kiitikadi wa tapo fulani la wanadamu. Kwa hiyo, kauli ya Baklu inatusaidia kupiga hatua ya kwanza katika kutanzua fumbo la nini “dunia” katika riwaya ya *Dunia Yao*, yaani kujua dunia ni nini kwa kubaini kile isichokuwa ndipo tuweza kusema kwamba kwa maana hii dunia mbili kinzani za Oyono ni sawa na dunia kadha wa kadha kinzani za Mohamed, ambazo hazina pahala mahsusi bali jumla ya mikondo ya fikra, falsafa na utendaji. Kugeukia kamusi kutafuta maana ya

dunia hizi kunaweza kutusaidia ama kuzing'amua barabara au kutupotosha kabisa.

Kamusi nyingi zinatoa fasili mbili kuu za neno “dunia,” moja inayoeleweka kwa mapana na marefu sana kama sayari na nyingine dhahania, isiyoshikika. Mathalani *Kamusi ya Kiswahili Sanifu: Toleo la Pili*, inaelezea maana ya kwanza ya dunia kuwa “sayari ambamo tunaishi” na maana ya pili kama “maisha.” *Kamusi la Kiswahili Fasaha* linatoa fasili ya kwanza ya dunia inayoshabihiana sana na ile ya *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, linaposema “dunia ni sayari tunayoishi ndani yake.” Lakini katika kueleza maana ya pili ya kamusi hili la visiwani, alikozaliwa mtunzi wa riwaya ya *Dunia Yao*, linasema dunia pia ni “mwenendo wa maisha.” Inabidi tuchague fasili safi na sahihi kati ya Kiswahili sanifu na Kiswahili fasaha. Tukichunguza matumizi mengi ya neno “dunia” nje ya maana ya sayari, twaona kuwa kusema dunia ni kisawe cha maisha kuna upungufu. Bora hapa tuchukue fasili ya *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Ingawa “dunia” hizi zinazotofautishwa na Oyono na Mohamed, sio sayari, na wala sio maisha tu bali ni mwenendo mzima wa maisha ya watu waliomo, na jinsi walivyoelekeana na *yaliyomo*, *yasiyokuwamo* na *wao kwa wao* na *wasiokuwa kama wao*. Hivyo dunia katika maana hii ni waliomo na yaliyomo na jinsi wanavyoonekana na wanavyojiona wenyewe.

Hata hivyo, ingawa mhusika wa Oyono, Baklu, anazungumzia dunia mbili kinzani, hapana shaka kwamba dunia anazorejelea mhusika Ndi— wa Mohamed ni dunia kadha wa kadha. Hapa ndipo hata mchoro mbele ya jalada la riwaya hii unavyozua utata. Mchoro wa sayari mbili katika jalada la *Dunia Yao*, unaashiria kuwapo kwa dunia mbili tofauti; moja ni sayari dunia yenye ramani ya bara la Afrika linaloonekana kupasuka nyufa kama mtungi unaokaribia kuvunjika wenyewe na dunia nyingine ndogo lakini iliyo juu na imara na yenye ramani ya mataifa ya Ulaya. Ni kweli kwamba kuwapo kwa kauli “dunia yao,” kunaashiria kuwapo kwa “dunia isiyokuwa yao.” Hivyo, kuzua dhana na uwezekano wa kuwapo dunia mbili kinzani. Lakini ufinyu huu wa maana ya dunia unaweza kutatiza zaidi badala ya kutanzua utata wa maana pana ya riwaya hii ya Mohamed. Ama kwa hakika, mchoro wa jalada unavyoashiria kwamba zipo dunia mbili tu unapotosha kwa kiasi fulani. Kwa hakika zipo dunia nyingi kwenye riwaya ya *Dunia Yao*, ambazo zimeainishwa kwa misingi mbalimbali kama vile viwango vya maendeleo ya kitaifa, matabaka ya kijamii, misimamo ya kiitikadi, maumbile ya jinsia na hisia, mtu alipo kinyakati, mtu aliposimama kipahala na kizazi chake mtu huyo.

Kuna dunia nyinginezo mbalimbali zisizokuwa dunia ya Ndi—. Kwa mfano, ipo dunia ya wafanyazi wenzake, mafisadi na wakandamizaji, dunia ya vijana wasiokuwa kama yeye, dunia ya wanawake isiyokuwa kama yake. Tunaweza

kuongeza kwamba utengano uliomo kwenye familia ya Ndi—kile Ndi—mwenyewe anakiita ukoo wake Ndi—umemfanya kila mhusika humo, si baba si mama si mtoto, kuwa kila mmoja katika dunia yake mwenyewe, ambapo kila mmoja anaandamana na mwenendo na msimamo wake mwenyewe. Hii ni taashira ya “dunia” anayoiwakilisha. Hapo pote neno “dunia” limetumika kwa maana ya “mwenendo wa maisha” kulingana na *Kamusi la Kiswahili Fasaha*.

Baklu hakabiliwi na utata kama wa Ndi— katika kuzitofautisha dunia zake mbili. Kwake Baklu kuna upande mmoja wa dunia ya weupe na mwenendo wao wa maisha yao (chambilecho *Kamusi la Kiswahili Fasaha*), na kuna dunia ya weusi na mwenendo wao wa maisha kwa upande mwingine. Hapa weupe wao na weusi sisi. Jambo la kusisitizwa hapa pia ni kwamba hata katika ufinyu wa mawanda madogo ya Kameruni ya kabla uhuru, uhuru ambao Ndi— wa Mohamed angeuita mageuzi tu, bado kuna mienendo ya maisha tofauti kati ya wenyeji, Waafrika na wakoloni, Wazungu ; mienendo inayoshadidia kuwepo kwa dunia mbili tofauti. Msimulizi wa Oyono, Toundi anatuwezesha kwa usimulizi wa masaibu makubwa yanayompata wakati anapojaribu kuikimbia dunia ya weusi na kuingia dunia ya weupe, kwamba kwa weupe hakuingiliki. Anaishia kufa kwa kipigo kikali cha mawakala wa serikali ya mkoloni (mweupe). Taswira ya dunia kinzani inajirudiarudia, na katika riwaya ya Oyono inajitokeza kama ukinzani kati ya dunia ya mweusi, mtendwa na mkandamizwa, na dunia ya mweupe, mtenda na mkandamizaji. Dunia hizi mbili ni kama lila na fila, hazitangamani.

Hii haimaanishi kwamba hapana mgawanyiko kati ya dunia ya weupe na dunia ya weusi katika riwaya ya *Dunia Yao*. Mgawanyiko huu ni ufunguo muhimu katika kuuelewa mwenendo na msukomo wa hadithi ya *Dunia Yao*, kufumbua kitendawili cha mkondo wa historia wa kuathiri na kuathiriana kati ya dunia ya weupe na dunia ya weusi, na jinsi mkondo huo unavyoamua hatma ya nchi Ndi— isiyokuwa na jina na aila yake Ndi— isiyokuwa na maana moja tu.

Tatizo moja kubwa linalobainishwa na *Dunia Yao* ni kwamba ipo tofauti kubwa kati ya dunia ya weupe na dunia ya weusi. Hapa ndipo tunapolazimika kuifasiri aila ya Ndi—kuwa ni zaidi ya aila tu bali isitiari ya taifa zima. Aidha, kile ambacho tunaweza kukiita taifa linalojidhania linaendelea mbele kumbe linarudi nyuma, limesimama, au limeanguka. Kama tutakavyoonyesha baadaye “kuendelea” ni neno la hatari sana, hasa ikizingitiwa ukweli kwamba mataifa ya Magharibi yaliyolibuni neno hilo “kuendelea” hayataki kwa dhati mataifa mengine yafikie viwango vya maendeleo sawa na yao. Yanataka pengo lidumu milele. Mwananadharia Fredric Jameson anatumia neno “Mataifa ya Ulimwengu wa Tatu,” maelezo ya kubishaniwa ambayo yanashadidia pengo kati ya dunia yao mbalimbali. Jameson anasema kwenye makala yake maarufu

ya "Third-World Literature in an Era of Multinational Capitalism," kwamba kinyume na fasihi toka Ulimwengu wa kwanza, fasihi kutoka Ulimwengu Tatu sharti iwe ni isitiari ya kitaifa. Jameson anafafanua kwamba kazi za fasihi za "Ulimwengu wa Tatu" hata zile ambazo yumkini ni za kibinafsi na zimebeba kabisa msukumo wa kiashiki, ni sharti ziwe na sifa ya kisiasa katika umbo la isitiari ya kitaifa; hadithi ya majaaliwa ya kibinafsi ya mtu mmoja pia ni isitiari ya hali yenye matata ya utamaduni na jamii ya umma wa ulimwengu wa tatu.

Kulingana na Jameson katika mataifa ya "Ulimwengu wa Tatu," hadithi ya mtu mmoja ni isitiari ya taifa zima, ni hadithi ya taifa zima. Hoja hii ya Jameson inaungwa mkono na kauli ya msimulizi Mwakote anayepokezana wajibu wa usimulizi na Ndi—katika *Dunia Yao* pale asemapo mwishoni mwa hadithi:

Ndi—akamweleza binti yake (Bisudi) hadithi yake mwenyewe Ndi—. Na hadithi ya Ndi—sasa si hadithi yake mwenyewe tu, bali ya jirani yake, na pia ya wananchi wenzake. Kwa kweli ni hadithi ya nchi yake. Hadithi mpya na kongwe. . . Na kwa njia hii ya kusimulia hadithi Ndi— alijizuia kufa. Kwa kuing'ang'ania sanaa mpya. Sanaa ya simulizi ya mdomo na maandishi. Sanaa mpya. Sanaa ya miujiza inayoelezea miujiza ya jamii (211).

Kwa kutuelekeza tuitazame hadithi ya Ndi— kama hadithi ya taifa zima, nchi nzima, Said A. Mohamed anatoa nadharia ya usomaji asahi (neni la Ndi—limaanishalo sahihi) wa fasihi ya aina anayoiandika. Vilevile anatoa vidokezo muhimu sana katika kuifasiri hadithi ya *Dunia Yao*. Hivyo riwaya ya *Dunia Yao* inajizungumzia yenyewe kinadharia, inajisoma yenyewe, inajihakiki yenyewe na kijifasiri yenyewe. Suala la riwaya kama hii kujitolea nadharia yenyewe si geni. Kama Olakunle George kwenye makala yake "*African Novels and the Question of Theory*," anavyoeleza kwa ufasaha na usahihi: "*many novels theorize themselves, initiating, in the grammar of their narrative fiction, how we might read them with profit.* [riwaya nyingi hujitolea nadharia zenyewe, zikituanzishia zenyewe kwa kaida zake za ubunaji wa kiusimulizi, jinsi tuwezavyo kuzisoma kwa manufaa]" (33).

Katika dondoo hili, riwaya hii ni changamano inajirejelea yenyewe inapozungumzia "sanaa mpya" anayoitumia Ndi—kumwelezea bintiye hadithi yake ambayo vilevile ni hadithi ya jirani na hadithi ya nchi yake. Hadithi hii ndiyo anasimuliwa Bisudi (jina linaloweza kumaanisha Bibi wa Sudi au Bahati). Nasi tayari tumekumbana nayo kufikia ukurasa huu wa mwisho wa riwaya. Tunaelewa kufikia hapa kwamba kazi hii inawakilisha "sanaa mpya" hasa kutokana na kuvuruga maana ya kawaida ya "uhalisia" kama tunavyoelewa. Kauli hii inatukumbusha kauli ya Ndi— mapema kwenye riwaya, adaipo: "Wakati wa sanaa ya uhalisia nilijua umeshapita" na badala yake umeingia uhalisiamazingaombwe (uk. 71). Lakini katika dondoo la

mwishoni mwa kitabu, mwandishi anatutolea sababu kuu ya kuwapo kwa hii “sanaa mpya” ya uhalisiamazingaombwe; “Sanaa ya miujiza, inayoelezea miujiza ya jamii.”

Amaanishacho ni kwamba jamii katika uhalisia wake wa sasa ina miujiza mingi mno kiasi kwamba njia mwafaka ya kuelezea au kuifafanua miujiza hii ni kutumia sanaa yenye miujiza. Hii ni sawa na kusema dawa ya moto ni moto. Tunashadidia kusema kwamba huu ndio utetezi mkubwa zaidi wa matumizi ya uhalisiamazingaombwe katika riwaya ya Kiswahili tuliowahi kuona. Ni katika kuelewa kwamba hii ni sanaa mpya (inayoafiki kufumbata uhalisia mpya), ndipo tupigapo hatua muhimu katika kulifumbua fumbo la dunia yao na yetu. Upya huu ni jambo la kubishaniwa ila lisitukwamishe hapa.<sup>2</sup> Kama anavyadai Said A. Khamis, mambo Afrika Mashariki ni mabaya mno kuweza kusimuliwa kwa uhalisia uliozoeleka tu. Wasanii, nyakati nyingine hulazimika kugeukia mbinu za majaribio, au “sanaa mpya” kama vile uhalisiamazingaombwe katika kujaribu kusawiri kizungumkuti cha hali halisi katika mataifa yao. Na kwa vyovyote vile, ipo haja kubwa ya hadithi kusimuliwa—ama kwa kinywa au kuandikwa, au kwa “mdomo na maandishi.” Kama msimulizi Mwakote anavyosema, ‘Ndi—anasimulia hadithi hii ili kujizuia kufa’. Hilo linaashiria haja ya kusimama kidete kwa nchi inayojidhanja kuwa inaendelea kwenda mbele kumbe inarudi nyuma, ili isimulie yenyewe au kuandika historia yake yenyewe, kuamua hatima yake yenyewe kwa sauti yake yenyewe. Kusimulia hadithi basi kunaambatana na kujitafiti na kujijua ili kuwa na sauti na uhuru kamili, sio “mageuzi” tu (chambilecho Ndi—). Ikiwa mataifa maskini hayana sauti, hayajisemei, yamedhibitiwa daima na nguvu kutoka nje, basi yamekufa kama Ndi— afapo hadithini. Katika hali hiyo ya kifo cha kimathali, haiwezekani “kuendelea” ila labda kuendelea kuoza na kuozeana.

Hali ya Ndi—, na ukoo wake na jirani yake na nchi yake ni duni hasa kutokana na nguvu kutoka nje—nje ya dunia yake, nguvu kutoka dunia nyingine, dunia yao. Chanzo cha hali mbaya hii ni kile Ndi—anachosema ni “lile dude linaloitwa “utandawazi” ambalo lipo kwa ajili ya manufaa ya mataifa ya Magharibi, au kama anavyosema Baklu katika riwaya ya Oyono, dunia ya weupe (148). Mataifa ya Magharibi, hasa kwa sasa Marekani inayotajwa kuwa “askari wa mataifa yote” (161). Marekani ni askari wa mataifa yote, ni kama kiranja wa mataifa kwa vile inadhibiti kila, kitu kila mahali duniani. Watu wa mataifa mengine wanakuwa kama Ndi—anavyoeleza: “Walikuwa kama masanamu ya roboti yaliyokuwa yakiendeshwa kwa ‘remote control’ na ‘gangstermkuu’ pahala fulani pa siri” (159).

Marekani ni “*gangster*mkuu,” jambazi jahili, tukitumia maneno ya Mohammed Said Abdulla. Mwandishi anatumia msamiati wa Kimarekani wa ‘*gangster*’ kuelezea maovu na makuru ambayo Marekani inayatekeleza inapohanjahanja ulimwenguni kama askari wa mataifa yote. Hiki ni kinaya kikubwa, kinyume kikubwa kwa mhalifu mkubwa zaidi kujiambika cheo cha kuwa askari wa mataifa yote. Ni kama paka kupewa kitoweo kulinda. Hapa Marekani ndilo “Jitu” (167-168) na “Jitukitu” (205-207) linalovua samaki, nao samaki ni mataifa maskini kama nchi ya Ndi—. Dhana ya kuvuliwa kwa nchi hizi kama samaki ni taashira ya kukosa hiari, kunaswa, kuathiriwa kwa mataifa maskini yanapokumbana na wimbi la ukandamizaji wa nguvu za Kimarekani na kiutandawazi ambazo kwa kiasi fulani ni kitu kimoja. Ndi—hata anaeleza utandawazi kama kisawe cha kuifanya dunia yote kukubali mtazamo wa Kimarekani, yaani “Americanization” ambapo mataifa yote yanalazimika kuimba “wimbo wa Washington” (175).

Hata hivyo, suala la mataifa maskini kudhulumiwa na kudhibitiwa, kuvuliwa kama samaki na kuendeshwa kama roboti zinazodhibitiwa kwa ‘*remote control*’ ni historia ndefu. Historia hii ya kuathiri na kuathiriwa inafungamana na uhusiano wa kinyonyaji kati ya dunia yao na dunia ya Ndi— dunia ya weusi na kile mwanafalsafa Charles Mills katika kitabu chake cha *The Racial Contract* anakiita “watu wasiokuwa weupe” Kama vile mhusika wa Oyono, Baklu, Mills anavyoainisha jamii ya wanadamu katika makundi mawili makuu. Kama inavyobainika hapa wazi, ingawa mawazo ya Mills yanaafikiana na ya Baklu kuhusu kuwapo kwa kundi la weupe kwa upande mmoja, yeye anasema kwamba ule upande wa pili una watu wasiokuwa weupe, kundi linalojumuisha wadhulumiwa wote.

Ndi— anaashiria kwamba mambo yalianza kwenda tenge kitambo katika enzi ya “wavumbuzi wa Kizungu” waliojiambika kuvumbua nchi na mabara na waliojiamulia wenyewe “jinsi ya kuumegea ulimwengu na kukatwa vipandevipande” (95). Kwa mujibu wa Mills kile ambacho mataifa ya Magharibi wamekiita “ziara za uvumbuzi” kwa kweli zilikuwa njama za mashambulizi ya kijeshi zenye lengo la kuyatiisha” mataifa mengine na kuyapunja. Kutiishwa huko kunadhihirika zaidi katika biashara za watumwa na baadaye ukoloni. Ilitumainiwa kwamba kuondoka kwa majanga haya mawili makuu, yaani utumwa na ukoloni, kungeleta unafuu. Lakini kama vile Ndi— anavyoeleza kuhusu kutoweka kwa ukoloni nchini kwake matumaini yaligeuka kuwa majonzi:

Hasama ikakua na kujaa ndani ya nafsi ya kila mtu. Ikawa haitoki milele. Hakuna mfano wake hapa Afrika Mashariki. Na mwisho kwa vishindo vikubwa zaidi, tukaiingia sisi, kunyakua utawala mpya na kuupaka rangi nyeusi—Mwafrika,

Mwafrika mtu mweusi, mtu mweusi! Mwanzo tuliimba kwa hoihoi. Mwisho tukalia machozi ya damu (148).

Kwa mara nyingine mwandishi anatumbea vipi tufumbue fumbo la dunia yao, yaani hadithi hii inahusu nani na wapi. Kutajwa moja kwa moja kwa Afrika Mashariki katika dondoo hili kunatuelekeza pahala mahsusi katika fasiri yetu ya mandhari ya hadithi hii.

Hadithi hii inahusu Afrika Mashariki na wakazi wake. Tunakumbana na maelezo haya ya mtamauko wa baada ya kuondoka mkoloni katika sura ya 13 ambayo mwanzoni mwanzoni Ndi—anasema “Niliamkia kuona mlango wa historia ya sasa u wazi” (147). Ni nini maana hasa ya historia ya sasa? Historia sio tu masimulizi ya mambo yaliyopita. Ninafikiri kwamba ipo “historia ya sasa” ingawa matukio ni ya awali, ya kitambo, lakini athari zake zipo sasa, wakati uliopo. Zamani na sasa hapana tofauti kubwa. Kisha Ndi—anaendelea kuelezea historia ya Afrika Mashariki ya kabla na baada ya ukoloni, historia ya hasama, na mafarakano, dhuluma, na migawanyiko ya kitabaka, kinasaba na kidini. Kuja kwa Waarabu na Uislamu, kuja kwa Wazungu na Ukristo kwa usingizio vya “kuudhibiti Uislamu usienee”(147) ilhali ashiki yao ya kutawala kama ashiki ya kingono ndiyo iliyokuwa sababu hasa ya kuja kwao.

Ndi—anakataa katakata kuuita uhuru hali ya baada ukoloni. Anasema: “Baada ya mageuzi (sipendi kuuita uhuru)”(16). Hili linaeleweka ukizingatia ukosefu wa hiari na mukhtari kwa mataifa ya Kiafrika ambayo yanadhibitiwa mno. Mambo yameenda kombo katika mataifa yaliyodhani kwamba yapo huru katika Afrika Mashariki kutokana na nguvu kutoka nje. Ndio maana baada ya msisimko wa siku za kwanza, wananchi wametumbukia katika majonzi na masikitiko makali sana ambayo usemi, “machozi ya damu” unawafaa sana kuyaelezea matatizo yao kwa msisitizo.

Kwa hiyo, hapa dunia yao inaweza kumaanisha Wamarekani na washirika wake wa Kimagharibi, na dunia ya Ndi— ni nchi maskini hasa hasa za Afrika Mashariki au jumla ya waathiriwa wa tamaa na ukiritimba wa Marekani. Mwandishi anajaribu kuelekeza Marekani na washirika wake kidole cha lawama kwa matatizo na masaibu yanazisibu nchi maskini. Hali ya Marekani kuwa chanzo kikubwa cha dhuluma inashangaza kwa maana awali Marekani yenyewe kihistoria ilikuwa mwathiriwa wa ashiki ya Ulaya, katika enzi ya uvumbuzi na kumegwa kwa ulimwengu na kukatwa vipandevipande. Mwindwa amekuwa mwindaji na hakuna kinachomzuia; na mojawapo ya mbinu yake muhimu ni kuwagawanya watu kwa sababu kwa maoni yake, “Kutawala maana yake ni kuwadunga watu sindano za sumu ya mafarakano” (98).



Kwa sasa mataifa maskini yakiwemo mataifa ya Kiafrika yako sawa na Ndi—mwenyewe kwa namna nyingi, yametindikiwa na uwezo wa kujitegemea, yamehasiwa, yanadunishwa na kujidunisha, yanaugua maradhi mbalimbali, yamezibwa kimya yasilalamike, yamekufa (tazama jinsi Ndi— anamwambia Bi Mize, “Kwa sababu mimi nimeshakufa), na chanzo cha hali hii chatoka kwingineko” (73)). Mtima anaondoka kwao ambako hana hakika nako tena kwenda Ughaibuni kwa sababu zilezile nguvu zinazotawala dunia zote, Ughaibuni na kule kuitwako Nyumbani, ila kwa mashaka. Nguvu hizi zinaamuliwa na kama asemavyo, Mtima bintiye Ndi—aliyekulia Uingereza, “lile dude liitwalo utandawazi: watawala wa dunia walio nje kabisa” (148) na lenye sifa za “Ki-Ungu”(149). Katika kukimbia kwao kwenda kutafuta ahueni ng’ambo, Mtima amekumbwa na nguvu za utandawazi ambao siku hizi umejaa nadharia tele za kujaribu kuufafanua. Hatuwezi kuyajumuisha mawazo mbalimbali kuhusu mada hii kutokana na muda na nafasi. Ila labda tuyazingatie mawazo ya mwanafalsafa Mnaijeria, Olufemi, Taiwo, anayelijadili suala hili kwa umahiri mkubwa katika kitabu chake, *How Colonialism Preempted Modernity in Africa*. Taiwo anaorodhesha sababu mbili kuu zinazowasukuma watu wa mataifa fukara kutaka kuhamia mataifa ya Magharibi. Yaani mvuto wa mataifa yaliyoendelea unaojidhihirisha kwenye vyombo vya habari na kuamsha hamu ya kawaida ya kibinadamu ya kutaka kuishi vizuri. Hoja kuu ya Taiwo ni kwamba nani hataki kuishi vizuri *apungu unyunyu akoye?* Anasema Taiwo:

*One the one hand, we have the normal, very human desire to always seek for the best life possible, and to go wherever there is some promise of a better life for us and our progeny. We cannot separate the current movements out of Africa into Europe and other parts of the world—there is at least one Nigerian businessman resident in Beijing—from the collapse of the economic mismanagement on a galactic scale by African “leaders,” and perhaps more important of all, the legacy of political repression, violence, and conflict (246).*

Kwa upande mmoja, tuna tamaa ya kawaida ya kutoka wakati wote maisha bora iwezekanavyo, and kwenda popote ambako kuna matumaini ya maisha bora kwetu na kwa uzao wetu. Hatuwezi kuitenganisha miondoko ya watu kutoka Afrika kwenda Ulaya na sehemu nyingine duniani—kuna angalau mfanyabiashara Mnaijeria mmoja mwenye makao yake Beijing— na mporomoko wa kiuchumi kwa kiwango kikubwa sana unaosababishwa na usimamizi duni wa “viongozi” wa Kiafrika, na muhimu zaidi urithi wa maonevu ya kiasia, fujo na mafarakano].

Kwake Taiwo utandawazi si jambo jipya sana kama watu wengine wanavyofikiria. Kwa msingi huu tunaweza kusema kwamba utandawazi umekuwa ukishamiri katika historia nzima ya uhusiano kati ya Mataifa ya Magharibi na Afrika. Anasema Taiwo:

*What is new under the sun globalization sun? The answer: little, if anything. It was Aristotle who said in ‘The Politics’ that humans are political animals: ‘zoon politikon’.*

*He forgot to add that we are also 'zoon dunamikon', animals that move around. And do we move around! If globalization is about anything at all, it is about movement, motion, dynamism—movements of peoples, ideas, services, kindness, vices, crimes and exploitation. (238)*

Nini kipya chini ya jua la utandawazi? Jawabu: kidogo, kama pana chochote. Ni Aristotle ndiye aliyesema kwenye kitabu chake cha *The Politics*, kwamba wanadamu ni wanyama wa kisiasa: *zoon politikon*. Alisahau kuongeza kwamba sisi pia ni *zoon dunamiko*, wanyama wanaotembeatembea. Nasi hutembea kweli! Kama utandawazi ni chochote, basi ni miondoko, kusongasonga, uendaji—miondoko ya watu, mawazo, huduma, huruma, maovu, uhalifu, na upunjaji.

Taiwo anatalia shaka madai ya mataifa ya Magharibi kwamba yanayatakia maendeleo na heri njema mataifa maskini. Ni kama vile anauliza je, aliye juu atatakea aliyeko chini aje juu pia? Haiyumkiniki.

### 3.0 Hitimisho

Tunahitimisha mjadala huu kwa kusema kwamba miito ya Mataifa ya Kimagharibi kuyataka mataifa mengine yashike maendeleo na demokrasia hauna ukweli ndani yake. Hayataki ushindani, na mataifa mengine yakiendelea yakayafikia, na hivyo yatakosa sababu ya kujinaki kwa kubakia kileleleni. Yaani kudamirika kama familia ya Ndi—au nchi ya Ndi— ni kwa masilahi ya madola hayo makubwa yanayotaka kuendelea kudhibiti mambo, kubaki kama vile Marekani, kiranja wa dunia na kujenga maadui. Kauli ya Ndi— kuwa “dunia yote imegeuka Magharibi” (45) ya kweli kabisa ukizingatia ukosefu wa usawa kati ya Magharibi na kwingineko. Labda anachomaanisha Ndi— ni kuzagaa kwa mikabala, mienendo, na mielekeo ya Kimagharibi. Kwa mfano, Yungi kufanya ukahaba na watalii wa Kizungu ni umagharibi wake. Lakini vinginevyo, utandawazi umezua chuki na uhasama miongoni mwa dunia yao (wa Magharibi) na kwingineko.

Tokeo mojawapo la chuki na uhasama zilizopandwa mbegu na *GangersterMkuu*, Marekani na washirika wake, ni kuibuka kwa “Pakashume” linalorejelewa kwenye riwaya hii na ambalo fasiri yake ni tishio la ugaidi ambalo limefungamana na imani kali za kidini pamoja na masilahi ya kitaifa na kifedha. Hata hivyo, Ndi—hasemi hivyo moja kwa moja ila anatoa mfululizo wa maswali ili kumwachia msomaji kuikatia kauli hali hii mwenyewe; anasema:

Mara ngapi namkumbuka pakashume anayetafutwa duniani kote. . . Yuko Amerika. . . Kajizika Afghanistan au Iraki. Mhusika wa visaasili pakashume. Mkononi gani uliomfanyanga? Vitendo gani vilivyomhamasisha? Kinywa cha nani kimemuumba? Nani kamjenga? Nani kambuni? Nini anachokamata yeye mwenyewe mkononi mwake? Pesa? Dini? Hamu ya kuua? Chuki kwa asili isiyokuwa yake? Heshima ya nafsi yake na watu wake (143).

Kwa namna fulani dondoo hili linathibitisha sifa mojawapo kuu ya riwaya hii ya *Dunia Yao* ambayo ni wingi wa maswali na uchache wa majibu. Hali hii inaashiria kutokuwapo kwa hakika ya chochote kuhusu mahali na nyakati, kweli anayoishadidia Ndi—asemapo: “Sikuwa na hakika ya chochote” (164). Usasa na usasabaadaye umesababisha kuyumbayumba na kuporomoka kwa dhana ya uhakika kwa chochote. Hakuna uhakika tena, hakuna uthabiti wa chochote, si watu si asasi si vitu.

Msomaji anapofikiria hasara iliyopatikana; mathalan kufarakana kwa aila ya Ndi—, kufa kwa Bori, na Kilua, na kuugua mshuko wa moyo kwa Mtima, anaweza kufikia kukata tamaa kwamba hapana matumaini kwa ukoo wa Ndi—. Kifo cha Kilua, anayedhamiria kuwa shujaa “Fumo Liongo wa Kike,” kinaonekana kuwa mwisho wa matumaini. Hili linauma sana kwa vile Ndi— aliyekwishatamauka kabisa, anadai: “Tamaa ilibaki kwa akina Kilua.” Mustakabali wa ukoo na nchi yake ulibaki katika kizazi kipya cha akina Kilua. Kwa kweli Kilua hafi kabisa, maana anazaliwa tena akiwa katika umbo la Bisudi. Lakini labda kuzaliwa kwa kitoto cha ajabu, Bisudi ndiyo taashira kubwa zaidi ya matumaini katika ulimwengu anaoubuni Mohamed katika riwaya yake ya *Dunia Yao*. Kwa hiyo, ni muhimu kuhitimisha kwa kutaja mwisho wenye matumaini katika riwaya hii.

Zipo dalili kadhaa za matumaini. Matumaini, mathalani yanajidhihirisha katika Yungi kuacha kufuata sera ya ufisadi na kuchuma hela halali. Ila labda dalili kubwa zaidi kwenye riwaya hii ni kuzuka kwa mwamko mpya wa wanawake kutaka kuitakasa dunia, kuifinyanga jamii yao au dunia yao. Ngoma ya kunguia anayochezwa Ndi— inatekeleza utakaso wa kitamathali kwa mwanaume na jamii yake nzima, ambamo wanawake sasa wameshika hatamu. Kama maiti hasa, Ndi— anaoshwa na kusafishwa ili awe na mwanzo mpya wa kupiga hatua za hakika kuelekea mustakabali ambao msingi wake ni maendeleo yanayotegemea ushirikiano baina ya wanaume na wanawake bila ubaguzi baina ya jinsia moja na nyingine au baina ya kizazi kimoja na kingine. Hili ni kinyume na kuwapo kwa dunia nyingi zinazowabaidi wahusika wa riwaya hii, dunia ya wanaume na dunia ya wanawake, dunia ya mafisadi na wasiokuwa mafisadi kama vile Ndi—, na dunia ya weupe na dunia ya weusi ambayo tumeiongelea kwa mapana na marefu. Ili kutanzua utata wa *Dunia Yao*, sharti tuanze kuiona aila ya Ndi—kama isitiari ya nchi inayojidhanja inaendelea, si hoja kama ni Zanzibar anakotokea mwandishi au ni nchi gani barani Afrika, na kwamba kila mhusika anawakilisha makundi fulani ya kiitikadi na kimwelekeo katika jamii. Hata hivyo, haimaanishi kwamba ni makosa kumwona Ndi—kuwa Ndiye Said A. Mohamed, kwa vile sio tu kwamba riwaya hii ina sifa za kitawasifu bali pia kwa sababu hakuna kitu awezacho mtu kuandika bila

kuchopeka ndani hadithi ya maisha yake. Kwa mantiki hii, *Dunia Yao* ni tawasifu ya Mohamed na Dunia yake na yetu.

### Tanbihi

1. Kistari katika jina la Ndi—ni ishara ya nakisi katika utu wa mhusika huyu. Amegawika kuwili. Anaweza kuwa kamili tu pale aunganapo na —Ye ili awe Ndiye, yaani kuingia katika ukamili wa utambulisho. Baadhi ya wahakiki kama vile Ken Walibora Waliaula wamekosea kwa kukipuuza kistari hicho katika uhakiki wao na maendelezo yao ya jina la Ndi—.
2. Katika kile anachokiita “uchambuzi wa uchokozi,” F.E.M.K. Senkoro kwenye makala yake ya “Uhalisiamazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili: Istilahi mpya, mtindo mkongwe,”(2007) anatilia shaka upya wa Uhalisiamazingaombwe katika fasihi ya Kiswahili. Senkoro aidahili kauli ya Khamisi kwamba mtindo wa uhalisiamazingaombwe ni mpya katika fasihi ya Kiswahili akidai kwamba kwake yeye istilahi tu ndiyo mpya ila mtindo huu wa kiusimulizi umekuwapo tangu riwaya za kwanza kabisa kuandikwa katika Kiswahili kama vile *Adili na Nduguze*, *Kusadikika* na *Kufikirika* za Shaaban bin Robert.

## Marejeo

- George, O. (2009). *African Novels and the Question of Theory. Katika Teaching the African Novel. Mhariri Gaurav Desai.* New York: MLA.
- Jameson, F. (1986). "Third-World Literature in an Era of Multinational Capitalism" katika *Juz. 15 uk. 65-88.*
- Khamis, S.M. (2005). "Signs of New Features in the Swahili Novel". *Research in African Literatures. Juz. 36/1 uk.92-108.*
- \_\_\_\_\_. (2007). "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili" *Kioo cha Lugha Juz. 5 11-23.*
- Mills, C. (1997). *The Racial Contract.* Ithaca, N.Y.: Cornell University Press.
- Mohamed, S.A.(2006). *Dunia Yao.* Nairobi: Oxford University Press.
- Oyono, F. (1976). *Boi.* Tafsiri ya Kiswahili ya Nathan Mbwele na Raphael Kahaso. Nairobi: Heinmann.
- Senkoro, F.E.M.K. (2000). "Uhalisiamazingaombwe katika fasihi ya Kiswahili: Istilahi mpya, mtindo mkongwe" *Kioo cha Lugha Juz.5 uk.1-10.*
- Taiwo, O. (2011). *How Colonialism Preempted Modernity in Africa.* Bloomington: Indian University Press.
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Waliaula, K.W. (2010).Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao The Tin Drum*" Katika *Swahili Forum* *Juz. 17 uk. 143-157.*